

Je, Chanjo za nyongeza za COVID-19 ni nini?

NAKALA

[Muziki wa kupendeza]

[Riwaya]

Baada ya mtu kupewa chanjo kamili, kawaida huwa na kiwango cha juu cha kinga dhidi ya COVID-19.

Takwimu mpya zinaonyesha kuwa kinga dhidi ya maambukizo ya COVID-19 hupungua kwa muda, hata kama chanjo zinaendelea kuwa nzuri sana katika kupunguza hatari ya ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini, na kifo.

Wakati kinga ya kwanza kutoka kwa chanjo inapoanza kupungua, chanzo ya ziada, inayoitwa chanjo ya nyongeza, inapeanwa kusaidia kuongeza kinga.

Kiwango hiki cha ziada hutengeneza kingamwili zaidi kumlinda mtu kutoka kwa ugonjwa.

Chanjo nyingi za kawaida zinahitaji nyongeza ili kudumisha kiwango cha juu cha ulinzi.

Kwa mfano, watu wanapaswa kupata chanjo ya pepopunda kila baada ya miaka 10. Chanjo hiyo ni nyongeza. "Inaongeza" uwezo wako wa kupambana na ugonjwa kwa sababu tunajua kinga hupungua kwa muda.

Kwa habari zaidi juu ya chanjo za COVID-19, nenda kwa health.mn.gov/covidvaccine.

[Muziki wa kupendeza]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

10/6/21 (Swahili)

Kupata habari hii kwa muundo tofauti, piga simu : 651-201-4989.